

Maswali na Majibu

1. Yesu aliambia wanafunzi wake wafanye nini?
Waambie kila mtu habari njema ya wokovu wa Mungu katika Yesu.
2. Yesu aliwambia kwamba atawapa nini ya kuwasaidia?
Nguvu ya Roho Mtakatifu.
3. Yesu alipeleka wanafunzi wapi? *Kwa Mlima wa Mizeituni.*
4. Nini ilifanyika kwa Yesu alipokuwa kwa Mlima wa Mizeituni?
Alipaa juu mbinguni.
5. Ni ujumbe gani yenye malaika wawili walipea wanafunzi?
Yesu atarudi hivyo hivyo mmemwona akienda.
6. Siku ya Pentekoste, nini ilifanyika kwa wanafunzi?
Upepo mkubwa ulikuja na ndimi za miale za moto zilituwa juu yao. Walipewa Roho Mtakatifu.
7. Wanafunzi waliweza kufanya nini baada ya kupewa Roho Mtakatifu?
Walizungumza lugha tofauti na kufanya miujiza. Waliandika Injili.
8. Petro aliambia umati nini?
Walisulubisha Yesu, Mwana wa Mungu, lakini ako hai tena.
9. Watu 3,000 walifanya nini siku hiyo?
Walitubu na wakabatizwa.
10. Mbona wanafunzi walihitaji Roho Mtakatifu?
Walikuwa na kazi nyingi ya kufanya, kuhubiri Injili kwa mataifa yote.

Mistari ya kukariri

Mathayo 28:19 – 20

Matendo 1:11

Matendo 2:36 – 37

Mazungumzo

Zungumza juu ya vile Roho Mtakatifu alisaidia wanafunzi kuhubiri Injili. Mbona hatuna Roho Mtakatifu sasa? Tunatumia nini kuhubiri sasa? (Biblia, maombi)
Zungumza vile tunaweza kuhubiri.

Kuandika

Andika juu ya nini ilifanyika siku ya Pentekoste. Petro aliambia watu nini iliyowaweka uoga. Walifanya nini juu ya hilo swala?

Masomo ya watoto wakubwa wa CBM



Somo la 39 Yesu anapaa Mbinguni

SOMA Mathayo 28:19 -20; Matendo 1:6 – 11; Matendo 2:1 – 41

SOMO

Wanafunzi walijua kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu, Masiya, aliyekuja kuokoa Waisraeli. Walijua kutoka kwa Agano la Kale kwamba Masiya atakuwa Mfalme na atatawala juu ya dunia yote.

Wanafunzi walikuwa wamemwona Yesu mara nyingi baada ya kufufuka. Walifurahi kwa sababu walijua yu hai tena. Walitarajia Yesu asimamishe ufalme wakati ule. Yesu alikaa nao kwa muda akiwaelezea juu ya unabii wa Agano la Kale. Aliwatayarisha kuhubiria watu habari njema ya Mungu na wokovu katika Yesu na Ufalme wa Mungu ujao.

Baada ya siku kama 40, Yesu alienda na wanafunzi wake mpaka Mlima wa Mizeituni ulioko nje ya Yerusalemu. Wanafunzi waliuliza Yesu kama atakuwa mfalme sasa. Yesu aliwajibu kwamba atakuwa mfalme wakati Mungu atamwambia iwe hivyo. Aliwambia waende waambia watu vile alikufa na sasa yu hai tena milele. Yesu aliwambia kwamba Mungu atawapa usaidizi. Mungu atawapa nguvu za Roho Mtakatifu iwasaidie kufanya kazi.

Yesu aliwambia kwamba kwa usaidizi wa Roho Mtakatifu, wataweza kuponya watu. Wataweza kutoa unabii na kunena kwa lugha zingine. Hii itawasaidia kwa kazi yao ya kuhubiri. Yesu aliwambia waende kwa watu wa nchi zingine. Walikuwa wabatize watu wote walioamini katika Yesu. Roho Mtakatifu itawasaidia pia kukumbuka mafundisho ya Yesu. Waliwezesha kuandika habari ya Injili kwa umakini sana.

Baada ya Yesu kusema haya yote alichukuliwa na kupaa mbinguni. Wanafunzi waliangalia akienda angani juu mpaka alipofunikwa na wingu. Walipokuwa bado wanachungulia juu, watu wawili waliokuwa wamevaa nguo nyeupe walitokea. Walikuwa malaika. Walizungumza na wanafunzi, “Enyi watu wa Galilaya, mbona mnasimama hapa mkiangalia angani? Huyu Yesu mwenye amechukuliwa kutoka kwenu kwenda mbinguni, atarudi hivyo hivyo kutoka kule mbinguni.”


Wanafunzi walitoka mlimani na furaha na kuridhika. Walijua Yesu ameenda mbinguni kuishi kule na Mungu. Malaika walikuwa wamewaahidi kwamba siku moja Yesu atarudi duniani kwa njia hiyo hiyo ameenda. Halafu atasimamisha Ufalme wa Mungu. Lazima waambie kila mtu hizo habari njema za wokovu katika Yesu Kristo. Wangeongoja kwa hamu kurudi kwa Yesu.

Yesu alikuwa amepea wanafunzi kazi nyingi ya kufanya. Yesu aliwambia waende waambie watu habari njema (Injili). Wanafunzi lazima waambie watu kwamba, Yesu amefufuka kutoka kwa wafu na atarudi kusimamisha Ufalme wa Mungu hapa duniani. Lazima waambie watu wabatizwe ili dhambi zao zisamehewe. Yesu aliambia wanafunzi waanze kuambia watu Habari Njema kuanzia Yerusalemu mpaka ulimwengu wote.

Yesu aliahidi wanafunzi kwamba atawatumia vipawa vya uwezo wa Mungu, Roho Mtakatifu. Nguvu za Mungu zitawasaidia kufanya miujiza. Hii itaonyesha watu kwamba, kweli Habari Njema ilitoka kwa Mungu. Roho Mtakatifu itawasaidia kunena kwa lugha tofauti. Hapo watu wataweza kuelewa ujumbe wao.

Wanafunzi walikaa Yerusalemu wakingoja Yesu awatumie Roho Mtakatifu. Siku ya Pentekoste, wanafunzi walikuwa pamoja wakiomba. Mara tu, kulitokea sauti kama ya upepo ikivuma kwa sauti kuu na kuingia kwa nyumba waliokuwa ndani. Waliona ndimi kama miale ndogo za moto na ikatua kwa kila mwanafunzi.

Wanafunzi wote walipata Roho Mtakatifu. Papo hapo walianza kuzungumza lugha tofauti. Kulikuwa na watu wengi Yerusalemu kwa sababu ya Siku kuu ya Pentekoste. Kulikuwa na Wayahudi waliotoka kwa nchi tofauti 17. Petro aliambia umati Habari Njema juu ya Yesu na Ufalme wa Mungu. Wayahudi wote wa kabila tofauti walielewe maneno yenye Petro alikuwa akisema.



Petro aliwambia kwamba ilikuwa uwezo wa Mungu wa Roho Mtakatifu uliowawezesha kunena kwa lugha tofauti. Petro aliwakumbusha juu ya miujiza yenye Yesu alifanya. Miujiza ilionyesha kwamba Yesu alikuwa Mwana wa Mungu. Walimsulibisha Yesu Mwana wa Mungu. Lakini Mungu alimfufua kutoka kwa wafu. Watu walikuwa na huzuni sana walipopata kwamba waliua Mwana wa Mungu. Waliuliza Petro wangepanya nini. Petro aliwambia kwamba, lazima watubu na wabatizwe, halafu Mungu atawasamehe. Karibu watu 3,000 walibatizwa siku ile.

Wanafunzi walihuri Injili Yerusalemu. Walifanya miujiza mingi kwa nguvu za Roho Mtakatifu. Hizo miujiza zilikuwa ishara kwamba mafundisho yao ilitoka kwa Mungu. Wanafunzi walifundisha watu kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu. Ni Masiya aliyetimiza ahadi za Mungu zote. Wanafunzi waliambia watu kwamba wanahitaji kutubu dhambi zao na wabatizwe. Kupitia kwa Yesu wanaweza kuokoka na kutoka dhambini ili waishi kwa Ufalme wa Mungu wakati Yesu atakuwa amerudi hapa duniani. Watu wengi waliamini na wakabatizwa. Kila siku watu waliamini kwa Yesu na kubatizwa.

ROHO MTAKATIFU

Mungu alipea wanafunzi Roho Mtakatifu kwa sababu ya kipekee. Walikuwa na kazi nyingi ya kufanya. Wanafunzi waliambia watu wa mataifa yote Habari Njema juu ya Yesu na Ufalme wa Mungu. Walihitaji usaidizi wa Mungu usio wa kawaida. Roho Mtakatifu aliwawezesha wanafunzi kuponya watu, kufufua wafu na kunena kwa lugha tofauti.

Mungu huwapa watu Roho Mtakatifu kama kuna kazi maalumu ya kufanya. Wanafunzi walifanya kazi yao kubwa na kueneza Injili kwa mataifa yote. Waliandika Injili ili sisi tuisome. Walipomaliza kazi yao, hakukuwa na haja ya kupea watu Roho Mtakatifu. Sasa, hatuna vipawa vya Roho Mtakatifu.